



Udhibiti wa Ada

Ulilipa ada ya matunzo ya watoto iliyo sahihi mwaka 2017?

Ni swala/jambo la haki kwamba wote walipe ada kwa ajili ya nafasi katika chekechea/kindergarten na sehemu ambayo mtoto anaendelea kucheza baada ya masomo shuleni /fritidshem.

Kuanzia Mwaka 2019 zinalinganishwa taarifa ambazo umepeleka kuhusu kipato/mshahara wako pamoja na taarifa ambazo umezipeleka katika maelezo ya mwaka mzima katika Mamlaka ya kodi. Kupitia udhibiti wa ada inaonyeshwa kama familia ililipa ada iliyo sahihi.

Endapo taarifa za kile kipato ambacho familia ilipeleka katika manispaa ya Säter ni pungufu kuliko kile ambacho familia ilitoa katika maelezo, hivyo familia itapata ankara/faktura ya ziada kutoka manispaa ya Säter. Familia itarudishiwa pesa iwapo ililipa ada ya juu zaidi.

Ankara/faktura zinatumwa mwezi Januari na inabidi kulipa kabla ya tarehe 31 Mars 2020.

Kwa wale ambao wanarudishiwa pesa wanapokea barua ambapo mtu anajaza taarifa za akaunti yake ili baadaye hizo pesa ziweze kuwekwa kwenye hiyo akaunti yake.

Udhibiti huo hufanyika kufuata uchelewesho wa miaka miwili kutokana na kwamba taarifa kutoka Mamlaka ya kodi zinakuwa hazipo kabla/mapema. Yahusuyo mwaka 2018 zitakuja kushughulikiwa mwaka 2020 na zitalipwa mwaka 2021.

Unapeleka taarifa mpya kuhusu taarifa za mshahara wako kupitia www.sater.se "E-tjänster" (inawezekana kupeleka kwa ajili ya mwezi unaofuata tu, hapana miezi iliyopita). Peleka mabadiliko yanapotokea kuhusu kipato/mshahara wako yanapobadilika ili kuepuka kuja kutakiwa kulipa baadaye.

Kwa taarifa zaidi angalia:

www.sater.se/barn-utbildning/förskola/avgiftkontroll

Wasalaam

Idara ya Elimu na Watoto

Manispaa ya Säter